

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU



Brazil

17 Novemba, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemuagiza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kuongoza timu ya ukaguzi wa majengo kukagua eneo lote la Kariakoo na kutoa hali ya taarifa kamili ya hali ya majengo katika eneo hilo mara baada ya zoezi la uokoaji kukamilika.

Aidha, Rais Dkt. Samia ameliagiza Jeshi la Polisi kupata taarifa kamili kutoka kwa mmiliki wa jengo lililoporomoka kuhusu namna ujenzi ulivyokuwa ukifanyika.

Rais Dkt. Samia ametoa maagizo hayo leo alipozungumzia tukio hilo lililotokea jana tarehe 16 Novemba 2024, ambapo ametoa rai kwa Watanzania wote kuungana kuwafariji wote walioguswa na tukio hilo.

Sambamba na hayo, Rais Dkt. Samia ametoa pole kwa wafiwa na ndugu, jamaa na marafiki wote walioguswa na tukio la kuperomoka kwa jengo hilo, na amewahakikishia wananchi kwamba kutakuwa na uwajibikaji.

Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa Serikali itagharamia matibabu ya majeruhi na kuhakikisha kuwa waliofariki katika tukio hilo wanasitiriwa ipasavyo.

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia amewapongeza vyombo vya usalama, watumishi wa afya, na wananchi wote walioshiriki zoezi uokoaji, na amempongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake wa zoezi hilo.

Rais Dkt. Samia anaendelea kufuatilia zoezi hilo, na ameeleza kuwa Serikali itaendelea kutoa taarifa za mwenendo wa zoezi la uokoaji.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

